



# HAKUNA UVUTAJI KWENYE MAENEO YA NJE MAHALI WANAPOLIA CHAKULA

Sheria Mpya inayozuia uvutaji kuanzia tarehe 22 Septemba 2010

## Marufuku uvutaji kwenye maeneo ya nje mahali wanapolia chakula hapa Western Australia

Mtu haruhusiwi kuvuta kwenye maeneo ya nje isipokuwa kama eneo hilo ndilo limetengwa mahususi kwa uvutaji.

**Eneo la nje kwa ajili kula chakula** ni eneo au sehemu ya eneo iliyotengwa kwa matumizi ya umma:

- lililotolewa, kwa misingi ya kibiashara, kuwa ni eneo ambalo watu wanaweza kukaa kwenye viti kwa ajili ya **kula chakula au kunywa**.
- si eneo la umma lililofungwa

Ni marufuku kuvuta katika eneo la nje kwa ajili ya kula chakula, ambapo watu wanakula na kunywa kipindi wamekaa mezani, kwa mfano kwenye migahawa, sehemu za kahawa, maduka madogo na sehemu nyingine za kununulia chakula.

### Sehemu yenye kibali cha kuuza pombe

Mtu mhusika (Mwenye mali/Mmiliki) wa kibali cha kuuza pombe ambacho hakipo chini ya leseni ya migahawa anauwezo wa kutenga sehemu yenye ukubwa wa kufikia 50% ya eneo la nje lililowazi kwa chakula kwa ajili ya wavutaji, hali mradi eneo hilo sio “eneo lililofungwa kwa matumizi ya umma”.

**Eneo la Uvutaji** ni sehemu iliyopo ndani ya mahali panapouzwa pombe kisheria ambapo:

- sio ndani ya jengo ambapo leseni ya biashara ya mgahawa inaruhusu,
- ni mahali nje palipo wazi ambapo wanaruhusu kula chakula, na
- ni eneo lenye ukubwa usiozidi 50% ya eneo lote la nje wanaporuhusu kula chakula.

Hatua za kutosha lazima zichukuliwe ili kuhakikisha kuwa eneo linaloruhusu watu kuvuta na kutokuvuta yanaonekana kwa uwazi nyakati zote. Hii ni kuhakikisha kwamba mipaka kati ya maeneo inafahamika kiurahisi kwa mtu aliyepo popote pale.

Mwenyemali/Mmiliki wa sehemu yenye kibali anashauriwa apunguze uwezekano wa wateja wao kuvuta moshi wa tumbaku na uvutaji ndani ya majengo yao kwa ujumla, ukijumuisha maeneo ya nje kwa ajili ya kulia chakula na wanaweza kuchagua kupiga marufuku uvutaji kwenye majengo yao.

### Alama ndani ya majengo yenye leseni za kuuza pombe

Sehemu zote ambazo haziruhusiwi kuvuta lazima zionyeshwe na alama iliyowekwa ukutani, kwa kutumia mabandiko ya kutosha na kuweka kwenye maeneo ambayo matangazo hayo yataonekana kwa mtu akiwa mlangooni sehemu ya kuingilia kwenye eneo hilo na ndani ya eneo hilo lililotengwa.

“Hakuna Uvutaji/No Smoking” au “Marufuku Uvutaji/Smoking Prohibited” au alama inayoonyesha hakuna uvutaji lazima ionyeshwe kama maelezo yanavyosema hapo juu.



Idara ya Afya itatoa alama stahili ili kusaidia biashara na Serikali za Mitaa ili kufikisha ujumbe huu wa kuzuia uvutaji.

## Wafanyakazi kwenye sehemu yenye kibali cha kuuza pombe

- Wafanyakazi kwenye sehemu yenye kibali cha kuuza pombe haitakiwi kushurutishwa kutoa huduma kwenye maeneo ya watu wanaporuhusiwa kuvuta na hawawezi kufukuzwa kwa kukataa kufanya hivyo.

## Hatua za Kisheria

- Serikali ya Mtaa inawajibu wa msingi kutekeleza hatua za kisheria zinazohusiana na kupigwa marufuku uvutaji ufukweni.
- Sheria mpya inaruhusu Halmashauri za maeneo kuchagua maofisa wa Afya au maofisa wa ziada, kwa mfano Rangers, ili kusaidia utekelezaji wake.

Ni muhimu kusisitiza kuwa sheria hii mpya inakubalika miongoni mwa jamii kwa kiwango kikubwa sana hivyo basi kutokana uzoefu wetu kutoka kwenye kipindi cha nyuma tunategemea kuwa wanajamii wengi wa Western Australia watafuata na kutekeleza.

## Adhabu

Kama kosa la uvutaji limefanyika ndani au kwenye gari pia kama kuna mtoto anaumri chini ya miaka 17 basi adhabu zifuatazo zinaweza kutolewa kwa mtu aliyefanya kosa hilo:

- |   |        |
|---|--------|
| ■ Mahakama inaweza kukupa amri ya kulipa faini ya kiwango kisichozidi | \$2000 |
| ■ Unaweza kupewa Notisi ya Kulipa                                     | \$300  |

## Majukumu ya Mwenyemali/Mmiliki

Mwenyemali/Mmiliki naye pia atakuwa ametenda kosa kama kuna mtu amefanya kosa la kuvuta kwenye eneo la nje kwa ajili ya kula chakula. Ili kuzuia usishtakiwe kwa kosa hilo Mwenyemali/Mmiliki lazima atoe ushahidi:

- walikuwa hawajui kuwa kosa hilo limefanyika, au
- kama wanajua kuwa kosa linafanyika, wamechukua hatua stahili kumzuia mtu huyo asivute.

Hatua stahili Mwenyemali/Mmiliki anaweza kuchukua zinajumuisha yafuatayo:

- kumfahamisha mtu huyo kuwa anatenda kosa
- kasha kumuomba aache kuvuta ndani ya eneo hilo, kuzima na kuitupa sigara
- kama mtu huyo atashindwa kufuata ombi hilo basi mwenyemali amuombe mtu huyo kuondoka kwenye eneo la wazi kwa ajili ya kula mpaka atakapomaliza kuvuta.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Tawi linalofuatilia Tumbaku:

Simu: 1300 784 892

Barua pepe/Email: [tcb@health.wa.gov.au](mailto:tcb@health.wa.gov.au)

### Disclaimer:

The information contained in this factsheet has been produced as a guide only. To view the full details in the relevant Tobacco Control legislation, visit [www.health.wa.gov.au/tobaccocontrol](http://www.health.wa.gov.au/tobaccocontrol)

